TANGAZO LA SERIKALI Na. 9 la Tarehe 3/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA KILIMO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA YA MWAKA, 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Afisa Ugani" maana yake ni mtaalam wa kilimo, mifugo, uvuvi na nyuki katika ngazi za Wilaya, Kata na Kijiji;

"mazao ya kilimo" maana yake ni mahindi, mbaazi, maharage, mtama, uwele, ufuta na mazao mengine;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Madaba;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika ambalo linanunua mazao ndani ya Halmashauri;

"muuzaji" maana yake mtu, kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika lolote linalojishughulisha na uzalishaji au uuzaji wa mazao ya kilimo ndani ya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni ushuru wa mazao ya kilimo unaolipwa halmashauri na mnunuzi wa mazao ya kilimo kutokana na kiwango cha ushuru kilichopangwa kwa zao husika.

"wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utaratibu maalum wa uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo

4.-(1) Halmashauri itaanzisha utaratibu maalumu wa uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo yanayopatikana na kuzalishwa ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Mazao ya kilimo yatauzwa au kununuliwa baada ya kukomaa na kuvunwa shambani na sio vinginevyo.

(3) Kila muuzaji au mnunuzi wa mazao ya kilimo anawajibika kuuza au kununua mazao ya kilimo na kutoza bei ya zao husika kwa mujibu wa bei elekezi itakayotolewa na Halmashauri na mamlaka husika.

(4) Kila zao la kilimo litauzwa, kununuliwa na kutozwa bei yake kwa kuzingatia kipimo cha mzani.

Leseni ya biashara ya mazao ya kilimo

5.-(1) Kutakuwa na leseni ya biashara ya ununuzi wa mazao ya kilimo itakayotolewa na Halmashauri.

(2) Kila mnunuzi wa mazao ya kilimo ndani ya Halmashauri atalazimika kuwa na leseni ya kuendesha biashara ya ununuzi wa mazao ya kilimo.

(3) Mnunuzi yeyote wa mazao ya kilimo kutoka nje ya nchi hataruhusiwa kununua mazao ya kilimo ndani ya Halmashauri bila kuwa na kampuni iliyosajiliwa Tanzania.

Kibali cha ununuzi wa mazao ya kilimo

6.-(1) Kutakuwa na kibali cha ununuzi wa mazao ya kilimo ambacho kitatolewa na Halmashauri.

(2) Mtu anayeomba kibali cha ununuzi wa mazao atapaswa kulipa ada ya kiasi cha shilingi elfu tano.

Wajibu wa Halmashauri

7. Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kuhakikisha kwamba inatoa vibali vya ununuzi na leseni za biashara ya

mazao kwa kila mnunuzi wa mazao ya kilimo ndani ya Halmashauri.

Wajibu wa Serikali ya Kijiji

8. Serikali ya Kijiji itakuwa na wajibu wa kufuatilia na kujiridhisha endapo mnunuzi wa mazao ya kilimo ana kibali halali cha ununuzi wa mazao ya kilimo na anazingatia matakwa ya Sheria ndogo hii.

Wajibu wa mnunuzi wa mazao ya kilimo

9. Kila mnunuzi wa mazao ya kilimo atakuwa na wajibu wa-

(a) kuwa na leseni ya kuendesha biashara ya ununuzi wa mazao ya kilimo itakayotolewa na Halmashauri;
(b) kuwa na kibali cha kununua mazao ndani ya Halmashauri;
(c) kununua mazao ya kilimo baada ya kukomaa na kuvunwa shambani na sio vinginevyo; na
(d) kulipa ushuru wa mazao kwa afisa mwidhiniwa au wakala mara tu baada ya kuyanunua.

Wajibu wa muuzaji wa mazao ya kilimo

10. Kila muuzaji wa mazao ya kilimo atakuwa na wajibu wa-

(a) kuuza mazao yake kwa mnunuzi mwenye leseni na kibali cha ununuzi wa mazao ya kilimo kutoka Halmashauri kwa kipindi cha mwaka husika anaonunua mazao; na
(b) kuuza mazao ya kilimo baada ya kukomaa na kuvunwa shambani na sio vinginevyo.

Hifadhi ya Mazao

11.-(1) Kila mkazi atakayelima shamba katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuvuna mazao yaliyokomaa na kuyahifadhi kwa njia salama.

(2) Kila mkazi atahakikisha kuwa anahifadhi chakula cha kutosha kwa angalau mwaka mmoja au zaidi.

(3) Kila mkazi atahakikisha kuwa ana ghala la kuhifadhia chakula ambalo ni imara na salama.

Vituo vya kuuza na ukaguzi wa

12.-(1) Halmashauri itaanzisha vituo mbalimbali kwa madhumuni ya kuuza na kukagua mazao ya kilimo yanayosafirishwa ndani na nje ya Halmashauri.

mazao ya kilimo

(2) Ukaguzi wa mazao ya kilimo katika vituo utahusisha uhakiki wa nyaraka za ununuzi wa zao husika, ushuru uliolipwa pamoja na vibali vilivyotolewa na Halmashauri kuruhusu ununuzi wa mazao husika yanayosafirishwa.

Usafirishaji wa mazao ya kilimo

13. Mtu yeyote atakayesafirisha mazao ya kilimo ndani au nje ya Halmashauri atahakikisha kuwa ana nyaraka zifuatazo:

(a) leseni ya biashara ya mazao ya kilimo iliyotolewa na Halmashauri;

(b) nakala ya stakabadhi ya ushuru uliolipwa na mnunuzi wa mazao hayo;

(c) vibali vya ununuzi wa mazao ya kilimo vilivyotolewa na Halmashauri kwa mnunuzi; na

(d) kibali cha kusafirisha zao husika.

Uteuzi wa Wakala

14. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa

15. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atauza au kununua, kuingia mikataba au makubaliano yoyote ya kuuza mazao ya kilimo yakiwa bado hayajakomaa shambani;

(b) atalazimisha kupita katika vituo vya ukaguzi wa mazao ya kilimo kwa nguvu bila kukaguliwa;

(c) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(d) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(e) ataendesha biashara ya mazao ya kilimo bila kuwa na leseni ya biashara iliyotolewa na Halmashauri; au

(f) atanunua mazao ya kilimo bila kulipa ushuru wa zao husika kwa Halmashauri.

Adhabu

16. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

17. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sita la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA KILIMO

1. Jina la Mnunuzi: ______________________________________________
2. Anuani S.L.P_____Mji/Kijiji_______Kitongoji___________Simu__________
3. Mahali anapoishi Mji/Kijiji___________________Kitongoji: ______________
4. Aina ya zao analotaka kununua: ________________________________________
5. Kiasi cha Mazao kinachonunuliwa: ____________________________________
6. Namba ya leseni ya biashara ya mazao ya kilimo_________________________
7. Kibali hiki kitaanza kutumika tarehe______________hadi tarehe____________

MIMI________________________________________ (Mnunuzi wa Mazao) NAAPA/NATHIBITISHA kwamba nitanunua mazao ya kilimo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ya Mwaka 2024 kwa kuzingatia kipimo cha kilo katika kutoza bei na sio vinginevyo. Ninatambua pia kuwa kununua mazao kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hiyo ni kosa na nitastahili adhabu.

Saini ya Mwombaji: _________________Alama ya dole gumba_______________
Tarehe ya kusaini kibali: ______________________________________________

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Maoni ya Afisa Muidhiniwa: Nakubali/ Nakataa kwa kuwa amekidhi /hajakidhi masharti ya Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ya Mwaka 2024.

Jina la Afisa Mwidhiniwa: ___________________________________________
Saini na mhuri wa ya Afisa Mwidhiniwa: __________________________________

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Madaba, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Kilimo ya mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru au ada ninayodaiwa kwa kiasi cha shilingi ……………….. pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi ………………………...

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe…………ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina………………………………..
Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina: …………………………………..……………
Saini……………………….…………………………
Wadhifa: ………………………………………………
Tarehe…………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na.9 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioketi katika ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Madaba tarehe 28/7/2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SAJIDU IDRISA MOHAMED,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Madaba*

TEOFANES TADEI MLELWA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Madaba*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Januari, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*